# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

## HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA KUSIMAMIA OFISI ZA VIONGOZI WAKUU WA KITAIFA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO , MAONI NA USHAURI YA KAMATI KWA OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA SERIKALI ZA MITAA NA IDARA MAALUM ZA SMZ KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

***************

**Mheshimiwa Spika,** awali ya yote naomba kuanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, kwa kutujaalia Uhai na Afya njema ambayo imetuwezesha kutekeleza vyema majukumu yetu ya kila siku. Vile vile, nachukua fursa hii kukushukuru wewe binafsi Mhe. Spika pamoja na wasaidizi wako kwa mnavyosimamia chombo hiki kwa uadilifu wa hali ya juu ili kufikia malengo ya Ilani ya Chama Cha Mapinduzi pamoja na Mipango mbali mbali ya Kitaifa katika kukuza Demokrasia.

**Mheshimiwa Spika,** napenda pia, kuchukua fursa hii kumshukuru na kumpongeza kwa dhati kabisa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa uongozi wake uliotukuka ambapo ndani ya muda mfupi tu wa uongozi wake tumeona mambo makubwa aliyowafanyia wananchi wetu na kila mmoja ni shahidi katika mageuzi makubwa ya kiuchumi na kijamii. Kamati inaridhishwa sana na juhudi za Mheshimiwa Rais pamoja na wasaidizi wake kwa kusimamia changamoto mbalimbali katika nchi yetu na kuzipatia utatuzi wake kwa wananchi. Kamati inamuomba Mwenyezi Mungu kumzidishia afya njema, hekma na busara katika kuitumikia nchi yetu na kupeleka mbele gurudumu la maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** pia, sina budi kumshukuru Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ Mhe. Massoud Ali Mohammed kwa uwezo wake na busara zake zilizomfanya apate mafanikio makubwa katika Ofisi hii pamoja na kuwapongeza watendaji wake wote wakiongozwa na Katibu Mkuu Ndugu Issa Mahfoudh Haji, Naibu Katibu Mkuu Ndugu Mikidadi Mzee Mwinyi, Wakuu wa Mikoa na Wakurugenzi wote ambao kwa kiasi kikubwa mashirikiano yao wanayotupatia ndio msingi wa mafanikio ya Kamati hii.

**Mheshimiwa Spika,** aidha, nitumie fursa hii kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati hii kwa ushirikiano wao mkubwa uliowawezesha kujadili ipasavyo na kuhoji mambo mbali mbali ambayo yametolewa ufafanuzi na Ofisi hii kwa lengo la kuhakikisha kwamba utekelezaji wa maoni/ushauri na mapendekezo yaliotolewa ndani ya ripoti ya Kamati yetu kwa mwaka wa fedha 2022/2023 chini ya Taasisi zake; utekelezaji wake umekuwa ni chachu ya maendeleo kwa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ lakini pia, katika kukuza na kuendeleza maendeleo ya nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,** kwa heshima na taadhima naomba sasa uniruhusu kuwatambua Wajumbe wa Kamati hii ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kama ifuatavyo:-

| | | |
|---|---|---|
| *1.* | Mhe. Machano Othman Said | Mwenyekiti |
| *2.* | Mhe. Mussa Foum Mussa | Makamu Mwenyekiti |
| *3.* | Mhe. Abadalla Abass Wadi | Mjumbe |
| *4.* | Mhe. Haji Shaaban Waziri | Mjumbe |
| *5.* | Mhe. Maryam Thani Juma | Mjumbe |
| *6.* | Mhe. Zaina Abdalla Salum | Mjumbe |
| *7.* | Mhe. Mwanaisha Mohammed Kheir | Katibu |
| *8.* | Nd. Ali Alawy Ali | Katibu |
| *9.* | Nd. Shawana Mohammed Haji | Katibu |

*10.* Nd. Amina Abeid Hemed Mkalimani

**Mheshimiwa Spika,** kwa kupitia Kanuni ya 107(3) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Toleo la 2020 Kamati zimepewa jukumu la kufuatilia utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati yaliyotolewa katika Ripoti ya Kamati ya mwaka uliotangulia; ambapo kazi hii ilifanywa vyema kwa kipindi hiki kilichopita na bado Kamati inazidi kufuatilia utekelezaji wa maoni hayo kila inapoona inafaa kufanya.

**Mheshimiwa Spika,** aidha, Kanuni ya *108(17)* ya Kanuni za Baraza, inaelezea kuwa kabla ya kuwasilishwa Barazani utekelezaji wa maoni na ushauri huo, Kamati inatakiwa kukaa na wizara husika ili kujadili utekelezaji huo unaojumuisha maoni na ushauri uliotolewa na Kamati dhidi ya wizara na taasisi zake.

**Mheshimiwa Spika,** Hotuba hii inaunga mkono utekelezaji wa maoni ya Kamati na inaelekeza kuwa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ imejitahidi kwa kiasi kikubwa katika utekelezaji wa majukumu hayo licha ya changamoto ndogo ndogo ambazo kimsingi utatuzi wake unafanyiwa kazi. Hata hivyo, jumla ya mapendekezo mia na sita (*106)* yaliagizwa katika Taasisi mbali mbali kupitia ripoti ya Kamati katika mwaka wa fedha 2022/2023 na jambo jema ni kuwa maoni hayo yamepatiwa majibu kutokana na utekelezaji wake ambao hadi sasa unaendelea. Aidha, Kamati inatoa ufafanuzi mchache tu wa baadhi ya hoja za maoni na ushauri uliotolewa kutokana na namna utekelezaji wake ulivyoibuka katika mjadala mbele ya Kamati.

**Utekelezaji wa Mapendekezo, maoni na ushauri wa Kamati kwa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imefarijika sana na inatoa shukurani zake za dhati kwa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa jinsi walivyoweza kutekeleza vyema maagizo hayo hali inayoonesha bidii katika utekelezaji wake pamoja na jitihada njema za kuleta maendeleo nchini.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa Ofisi imetekeleza vyema maoni na ushauri uliotolewa na Kamati ndani ya kipindi kifupi cha miezi sita, lakini bado kuna baadhi ya maoni na ushauri ambao Kamati imeitaka Ofisi kufuatilia zaidi utekelezaji wa maoni hayo kwa kutoa maelekezo yafuatayo:

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imeshauri Mamlaka ya Serikali za Mitaa kuandaa programu maalumu ambayo itawasaidia kupata vyombo vya usafiri kwa urahisi kutokana na changamoto za usafiri kwa Halmashauri zote za Unguja na Pemba. Kamati imeelezwa kuwa malengo ya Serikali kuu ni kuwa na mpango wa jumla wa kuzipatia ofisi zote za Mikoa na Serikali za Mitaa magari.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imeishauri Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kupitia Mamlaka ya Tawala za Mikoa kuendeleza juhudi za kupambana na makundi hatarishi yanayojitokeza katika jamii ili kulinda na kuendeleza amani kwa wananchi wetu na wageni. Kamati imeridhishwa na utekelezaji wa ushauri huu kwa namna wanavyopambana na makundi maovu na kulinda usalama wa wananchi na wageni. Aidha, Kamati imeitaka Ofisi kuonesha katika majibu yake hatua zilizochukuliwa kwa wahalifu waliopatikana na hatia pamoja na hukumu iliyotolewa ili iwe ni funzo kwa vijana wengine ambao wanajihusisha na makundi kama haya.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati pia, ilishauri Serikali kujenga Ofisi za Wakuu wa Wilaya ili kupata makaazi bora pamoja na kuzikarabati nyumba wanazoishi au kujengwa upya pale ambapo uwezo utaruhusu. Kamati imeridhika na majibu ya Ofisi hii kutokana na mipango ya Serikali kuhusu ujenzi wa Afisi za Wakuu wa Wilaya pamoja na Masheha sambamba na ukarabati wa nyumba za Wakuu wa Mikoa na Wilaya. Hata hivyo, Kamati imeitaka wizara kuainisha ni wakati gani ambao Ofisi za Masheha zitaanza kujengwa ili kuweka bayana kwamba mpango huu na utatekelezwa kama ulivyopangwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati kupitia ripoti ya mwaka 2022/2023 imebaini kuwepo kwa fungu dogo la bajeti kwa Ofisi za Wakuu wa Mikoa husuan Mkoa wa Kaskazini Pemba, jambo ambalo tulishauri Ofisi kufanya maombi maalumu na kuyawasilisha Ofisi ya Rais

Fedha na Mipango ili kupatiwa nyongeza ya bajeti. Hata hivyo, Kamati haikuridhishwa na majibu ya ushauri huu na hivyo, kuiomba wizara kufuatilia moja kwa moja suala hili na kutoa ufafanuzi wa kina na hatua zilizochukuliwa katika utekelezaji wake.

**Mheshimiwa Spika,** katika ziara zake mbali mbali za Kamati kwenye Halmashauri imekuwa mstari wa mbele katika kuwashajihisha wajasiriamali kujisajili na kupatiwa vitambulisho kupitia Ofisi za Manispaa na Mabaraza ya Miji, jambo ambalo utekelezaji wake hauko katika hali mzuri. Sambamba na hayo, Kamati imeishauri Manispaa ya Mjini kuhakikisha limeendeleza zoezi la wajasiriamali pamoja na kuwapatia vitambulisho vya kazi kwa mujibu wa maeneo yao ili kupunguza vijana wanaozurura mitaani. Aidha, Kamati inatoa wito kwa Halmashauri, Mabaraza na Manispaa zote kuhakikisha wamefuatilia na kutoa vitambulisho vya wajasiriamali katika maeneo yao, kwa mnasaba wa kuwatambua na kuwapangia maeneo ya kibiashara ambayo yametayarishwa kwa ajili yao.

**Mheshimiwa Spika,** vile vile, katika kuweka mji safi na wenye haiba nzuri kupitia vyombo vya usafiri katika maeneo mbali mbali; Kamati inashauri Serikali kupitia Mamaka ya Serikali za Mitaa kutoa fursa kwa wawekezaji kuekeza katika ujenzi wa maegesho ya magari ili kupunguza msongamano wa magari pembezoni mwa barabara pamoja na kusaidia kuongeza vyanzo vya mapato kwa Mamlaka hizi.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Idara Maalumu za SMZ Kamati yangu imeridhishwa sana na utekelezaji wa maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati kupitia ripoti hii, jambo ambalo limetoa sura mzuri katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku. Hata hivyo, Kamati inaendelea kuzishauri Idara hizi kujiwekea utaratibu wa kuandika miradi ya maendeleo na kuitafutia ufadhili wa kuiendesha miradi hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** Aidha, Kamati inashauri Jeshi la Kujenga Uchumi pamoja na Chuo Cha Mafunzo Zanzibar kutafuta miradi ambayo itawasaidia katika kilimo cha umwagiliaji ili kupambana na mabadiliko ya tabianchi ambapo kwa kiasi kikubwa harakati za kilimo zimefifia katika Idara hizi kutokana na ukame unaowakabili kila

sehemu.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kumalizia Kamati inaishauri Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ Kuzisimamia vyema Halmashauri za Wilaya, Mabaraza ya Miji na Manispaa ili kuhakikisha wameongeza nguvu maalumu katika kufanya usafi wa miji na kuibua vyanzo vipya vya ukusanyaji wa mapato. Mbali na hayo, Kamati inaziomba Mamlaka hizi kuhakikisha masoko ya wajasiriamali yamekamilika na kuondoa changamoto ndogo ndogo ambazo zimeibuka kwa baadhi ya masoko.

**Mheshimiwa Spika,** mwisho kabisa, naomba kuchukua fursa hii tena kuishukuru Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kuipitia viongozi wake kwa mashirikiano makubwa wanayoipatia Kamati katika kutekeleza majukumu yake na kuomba kuzidisha mashirikiano hayo ili kufikia malengo ya nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha.

Ahsante,

.................................

(Mhe. Machano Othman Said),

**Mwenyekiti,**

**Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa,**

**BARAZA LA WAWAKILISHI,**

**ZANZIBAR**